

Jinsi ya Kufanya Kipimo cha COVID-19 cha Lucira Check It

HATUA YA 1. Chukua kipimo katika eneo la upimaji.

HATUA YA 2. Kagua maelekezo yote yanayohusiana na kipimo.

HATUA YA 3. Jipime nje ya eneo la huduma na usubiri kwa dakika 30 kupata matokeo yako.

HATUA YA 4. Ripoti matokeo katika healthvermont.gov/reportresults na ujaze fomu fupi.

Ni muhimu kuripoti matokeo ya kipimo chako. Jibu lako ni siri.



HATUA YA 5. Iwapo uthibitisho wa matokeo ya kipimo unahitajika, tuma neno 'LUCI' kwenda 44544 na fuata maelekezo zaidi.

Kwa maagizo yaliyotafsirwa ya upimaji na video za maagizo tembelea

<https://www.healthvermont.gov/covid-19/testing#testdetails>
[QR CODE]

Kipimo cha COVID-19 cha Lucira Check It kinakuja na **betri 2 za AA**.

Tafadhalii zingatia kutumia tena au kurejeleza betri hizi kulingana na miongozo ya mamlaka ya eneo ya uchafu usio oevu baada ya matumizi.

Maswali Yanayouulizwa Sana

Je, kipimo cha COVID-19 cha Lucira Check It ni cha aina gani?

LAMP ni aina ya ukuzaji wa molekuli ambayo hutumiwa katika kipimo cha Lucira. Kama ilivyo kwa vipimo nya PCR nya maabara, kipimo cha Lucira hukuza nyenzo za kijeni za virusi nya SARS-CoV-2 wakati kipimo kinaendelea. Ukuzaji unaotokea katika kipimo cha PCR na Lucira huwezesha vipimo nya maabara kugundua sampuli chanya. Kwa hivyo, usahihi wa Lucira unalinganishwa na mojawapo ya vipimo nya maabara nya PCR nya usahihi wa juu zaidi.

Je, Kipimo cha COVID-19 cha Lucira Check It kinalinganishwa vipi na Kipimo cha PCR?

Vipimo nya maabara, kama vile kipimo cha PCR na Lucira, hunakili nyenzo za kijeni za virusi mara kwa mara wakati kipimo kinaendelea katika mchakato unaoitwa ukuzaji. Hii inawezesha vipimo nya maabara kugundua ikiwa mtu ana virusi nya SARS-CoV-2 wakati kuna kiwango kidogo tu cha virusi.

LUCI Pass ni nini?

LUCI Pass ni bidhaa ya Lucira yenyewe kurahisisha kupokea matokeo ya kipimo cha Lucira bila malipo, yaliyothibitishwa kidijitali kwenye simu yako mahiri. Baada ya kufanya kipimo chetu, unatuma tu neno "LUCI" kwenda 44544 au unaenda katika luci.lucirahealth.com kwenye simu yako ili kufikia tovuti yetu kuu salama ya LUCI, kisha unafuata hatua chache ili kuwasilisha matokeo yako.

Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa matokeo yangu ya kipimo ni chanya?

Iwapo utathibitishwa kuwa na virusi, hakikisha kuwa umeripoti matokeo yako kuititia kiungo kilichopo upande mwingine wa kadi hii. Kwa mwongozo wa ziada, tafadhalii tembelea healthvermont.gov/covid19positive

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu Kipimo cha COVID-19 cha Lucira, nenda kwenye checkit.lucirahealth.com